# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara ya Uchaguzi wa Burlington

## Najisajili Vipi ili Kupiga Kura? Makataa ni Gani?

Unaweza kujisajili ili kupiga kura wakati wowote kuanzia sasa hadi Siku ya Uchaguzi. Una chaguo chache za usajili:

- Mtandaoni: Tembelea olvr.vermont.gov/
- Fomu ya Karatasi: hii inaweza kuletwa kwa Ofisi ya Karani/Mwekahazina wa Burlington au kutumwa kwa posta sos.vermont.gov/media/nesb43yw/2017-voter-app.pdf
- Mtu mwenyewe: Nenda kwenye Ofisi ya Karani Mwekahazina, 149 Church Street, Burlington, VT 05401. Piga (802) 865-7000 katika saa za ofisi.
- Siku ya Uchaguzi: Katika eneo la kupiga kura kwa wilaya wako wa kupiga kura (au “wadi”)

Ikiwa unajisajili kupiga kura katika Vermont kwa mara ya kwanza kupitia posta au mtandaoni, lazima ujumuishe nakala ya aina ya kitambulisho inayokubalika. Aina za kitambulisho zinazokubalika ni:

- Picha halali ya kitambulisho (leseni ya dereva au pasipoti)
- Bili ya sasa ya matumizi
- Taarifa ya benki ya sasa
- Waraka mwingine wa serikali

## Nathibitishaje kuwa Nimesajiliwa Kupiga Kura?

Tafuta Orodha ya Ukaguzi wa Wapiga Kura katika Burlington kwenye tovuti ya Katibu wa Jimbo la Vermont katika mvp.vermont.gov ili kuthibitisha usajili wako na wilaya ya kupiga kura (au wadi), ikiwa umesajiliwa, itakupatia pia maelekezo ya kukupeleka katika eneo lako la kupiga kura. Ikiwa hujasajiliwa, unaweza kujaribu tena mapema kwa njia zilizoorodheshwa hapo juu, au unaweza kujisajili kupiga kura katika eneo lako la kupiga kura Siku ya Uchaguzi.

## Napigaje Kura?

- Tuma kura yako kwa Ofisi ya Karani/Mwekahazina
- Leta kura yako katika eneo la kuweka kura
- Wewe mwenyewe Siku ya Uchaguzi

Una chaguo la kupiga kura mapema, lakini unaweza pia kuchagua kwenda katika eneo lako la kupiga kura Siku ya Uchaguzi. Wasiliana na Ofisi ya Karani/Mwekahazina ili kupata maelezo kuhusu jinsi ya kupata kura yako uliyokosa.

**Maagizo ya Kurejesha Kura**

1. Piga kura kwenye karatasi yako ya kupiga kura. Tafadhali fuata maagizo katika sehemu ya juu ya karatasi ya kura ili kufanya uteuzi wako. Ikiwa unatumia sampuli ya kura iliyotafsiriwa ili kufanya

marejeleo, LAZIMA UANDIKE MAJIBU YAKO KWENYE KURA YA TOLEO LA KIINGEREZA. Majibu yaliyoandikwa kwenye sampuli ya kura hayatakubaliwa.

2. Weka kura yako iliyokamilika ndani ya Bahasha ya Kura Iliyopigwa.
3. Chapisha jina lako na Jiji katika nafasi zilizotolewa mbele ya Bahasha ya Kura Iliyopigwa.
4. WEKA SAINI KWENYE CHETI! LAZIMA USAINI kwenye Bahasha ya Kura Iliyopigwa, au KURA YAKO HAITAHESABIKA.
5. Funika Bahasha ya Kura Iliyopigwa ikiwa na kura yako ndani.
6. Weka Bahasha ya Kura Iliyopigwa ndani ya barua ya posta iliyolipiwa mapema iliyoelekezwa mapema kwa Karani wa Jiji. Unaweza kuandika anwani yako ya kurejeshwa/nyumbani kwenye sehemu ya juu ya upande wa kushoto.
7. Rudisha kura yako kwa posta, katika eneo la kisanduku cha kuweka kura, katika Baraza la Jiji saa za biashara, au katika eneo lako la kupiga kura Siku ya Uchaguzi.
8. Ikiwa unatuma kwa posta, tafadhali ruhusu siku 7-10 za biashara ili Ofisi ya Karani iweze kuipokea.

**Maelekezo ya Kupiga Kura Mwenyewe katika Kituo**

1. Fika katika eneo lako la kupiga kura na upange foleni, leta kura yako uliyotumiwa ikiwa uliipokea. Kwa kawaida muda wa kusubiri ni fupi lakini unaweza kuwa ndefu wakati wa uchaguzi wa rais. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kupiga kura, umeruhusiwa kuleta mtu mmoja uliyemchagua ili akusaidia kwenye mchakato huo.
2. Ukifika kwenye meza, taja jina lako vizuri. Waambie wafanyakazi wa uchaguzi jina lako la mwisho au jina la familia kwanza. Ikiwa kwa sababu yoyote hawawezi kukupata katika orodha yao ya wapiga kura waliosajiliwa, watakutuma kwa meza nyingine ili kujaza fomu zako za usajili kabla ya kuweza kupiga kura. Ikiwa ulitumiwa barua kupitia posta na hukuileta, wanaweza kukuomba kusaini hati ya kiapo inayothibitisha kuwa bado hujapiga kura kabla ya kuweza kupokea kura.
3. Leta kura yako katika kisanduku cha faragha. Ikiwa inahitajika, unaweza kurejelea sampuli ya kura zilizotafsiriwa (https://www.burlingtonvt.gov/CT/Sample-Ballots-Warnings-and-Notices) huku ukijaza kura ya Kiingereza. MAJIBU YOTE LAZIMA YAJAZWA KWENYE KURA YA KIINGEREZA, sampuli ya kura zilizotafsiriwa haziwezi kuwasilishwa.
4. Mara tu umekamilisha uteuzi wako, utaleta kura yako iliyokamilishwa kwenye mashine ya kupiga kura, na mfanyakazi wa uchaguzi atakusaidia kukihitajika. Mara hii imekamilika, kura yako imewasilishwa na unaweza kuondoka.

Unatafuta video za maagizo? Tazama maagizo katika Kiingereza, Kisomali, Kiswahili, Kinepali, Kifaransa, Kiburma na Kiarabu katika https://www.youtube.com/channel/UCdy2e0EwW59oMye-Odnh3rQ/featured/.

## Nitajuaje Kuwa Kura Niliyotuma kwa Posta Ilihesabiwa?

Unaweza kufuatilia hali ya kura yako kwenye mvp.vermont.gov/ ili kujua kuwa ilipokelewa na karani wa mjiji wako.

## Makataa ya Kutuma Kura Yangu ni Gani?

Kura lazima iwasilishwe kwa karani wa mji wako kufika 4:30 Jumatatu kabla ya Uchaguzi au kwa kura kati ya 7AM na 7PM Siku ya Uchaguzi.

## Naweza Kupiga Kura Wapi Mimi Binafsi Siku ya Uchaguzi?

Unaweza kutafuta anwani yako ya nyumbani katika www2.burlingtonvt.gov/Clerk/Elections/Map/ ili kupata ni wadi gani (au wilaya ya kupiga kura) unastahili kuwa. Pia tumejumuisha ramani ya sasa ya wilaya ya kupiga kura yenye ikoni zinazoonyesha kila eneo la kupiga kura. Maeneo ya kupiga kura katika Burlington ni:

**Wadi 1**

Mater Christi School
100 Mansfield Ave

**Wadi 2**

Integrated Arts Academy katika H. O. Wheeler School
6 Archibald Street

**Wadi 3**

Lawrence Barnes Elementary School
123 North Street

**Wadi 4**

Saint Mark's Youth Center
1271 North Avenue

**Wadi 5**

Burlington Electric Department
585 Pine Street

**Wadi 6**

Edmunds Middle School
275 Main Street

**Wadi 7**

Robert Miller Community & Recreation Center
130 Gosse Court

**Wadi 8**


Fletcher Free Library
235 College Street

**Kwa maelezo au mwongozo zaidi wasiliana na Ofisi ya Karani/Mwekahazina katika:**

149 Church Street
Burlington, VT 05401
(802)-865-7000
**www.burlingtonvt.gov/CT/Elections**

**Maelezo ya Uchaguzi wa Vermont:**

**https://sos.vermont.gov/elections/election-info-resources/**


City Council
Wards and Districts
Burlington, Vermont
Effective March 3, 2015
Wards:
1
2
3
4
5
6
7
8
District Boundary
Voting Location
Derway Island
COLCHESTER
Winooski River
WINOOSKI
SOUTH BURLINGTON
STARR FARM RD
NORTH AVE
STANIFORD RD
ETHAN ALLEN PKY
VT 127
NORTH AVE
Leddy Park
Appletree Point
Appletree Bay
BHS
North Beach
Lone Rock Point
Intervale
NORTH ST
PEARL ST
RIVERSIDE AVE
COLCHESTER AVE
EAST AVE
UVM
MAIN ST
Gorge Island
BATTERY ST
MAIN ST
MAPLE ST
SO PROSPECT ST
PINE
ST PAUL ST
SHELBURNE ST
FLYNN AVE
HOME AVE
Oakledge Park
Red Rocks Park
Juniper Island
Lake Champlain
Burlington Bay
Burlington GIS